


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA



**Unapojibu tafadhali taja:**

**Kumb. Na. BDC/D.10/4/7/8**

12 Machi, 2022

**YAH:TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA KUKUSANYA TAARIFA ZA ANWANI ZA  
MAKAZI(POSTI KODI) NAFASI 200.**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega anapenda kuwatangazia nafasi za ajira ya muda kwa nafasi za wakusanya taarifa kwenye zoezi la anwani za makazi katika kata na vijiji vyote vya Halmashauri ya Wilaya ya Busega.

**A. SIFA ZA MWOMBAJI**

- i. Awe raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18-35.
- ii. Awe na elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea.
- iii. Awe anamiliki simu janja(smartphone)inayotumia mfumo wa Android na yenye uwezowa kukaa na chaji kwa siku nzima.
- iv. Awe na uwezo wa kutumia simu janja kutengeneza taarifa mbalimbali zilizomo kwenye simu (word na excel).
- v. Awe na barua pepe (email address) inayofanya kazi.
- vi. Awe ni mkazi wa kata husika anayoomba.

**B. KAZI NA MAJUKUMU**

- i. Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma
- ii. Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, viwanja na maeneo ya huduma kwa kutumia mfumo wa anwani za makazi.
- iii. Kutumia data kwenye mfumo wa anwani za makazi.
- iv. Kazi hii itafanyika kwa muda wa siku zisizozidi 10.
- v. **Malipo yatafanyika kwa kuzingatia kiasi cha kazi kwa siku.**

**C. MAOMBI YAAMBATANISHWE NA:**

- i. Nakala ya cheti cha kidato cha nne na kuendelea.
- ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
- iii. Picha (Passport size 2).
- iv. Barua ya maombi ipitie kwa mtendaji wa kijiji au kata anapoishi.

**D. JINSI YA KUTUMA MAOMBI.**

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya mwombaji, namba yasimu na barua pepe; Maombi yawasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega kwa anwani ifuatayo:-

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA  
S.L.P 157  
BUSEGA**

**E. TAREHE YA MWISHO YA KUPOKEA MAOMBI.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 15/03/2022 saa 9:30 Alasiri.



.....  
Veronica Vicent Sayore  
Mkurugenzi Mtendaji

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA.**